MAFUNZO YA WALIMU KAZINI NGAZI YA SHULE
KWA MWALIMU WA DARASA LA I-III

Moduli ya Nane:

FONIKI

Mwongozo wa Mratibu wa Mafunzo ya Walimu Kazini Ngazi ya Shule

UKaid
from the British people

equip Tanzania
Education Quality Improvement Programme

Moduli hii imetayarishwa kwa ushirikiano na:

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi
Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
Taasisi ya Elimu Tanzania
Chuo Kikuu cha Dodoma
Chuo cha Ualimu Morogoro
Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam
Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa
EQUIP-Tanzania

Moduli hii imewezeshwa kwa ushirikiano na:

C.C.U Butimba
C.C.U Bustani
C.C.U Tabora
C.C.U Ndala
C.C.U Kasulu
C.C.U Kabanga
C.C.U Bunda
C.C.U Tarime
C.C.U Shinyanga
C.C.U Mpwapwa

DIBAJI

Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, imetoa kipaumbele katika sekta ya elimu ili kuleta mageuzi ya kiuchumi na kijamii. Lengo la Dira ya Maendeleo ni kuwa na taifa la watu waliolelimika na jamii iliyo tayari kujifunza kufikia 2025. Serikali ya Tanzania imethibitisha kwa vitendo kuwa Elimu ni kiambato muhimu katika kupunguza umaskini na kuimarisha maendeleo ya taifa. Kwa muda mrefu serikali imetambua kuwa "Ubora wa Elimu yoyote hauwezi kuwa bora kuliko mwalimu mwenyewe" hivyo imetilia mkazo mafunzo kazini kwa walimu kupitia mikakati mbalimbali ili kuimarisha umahiri wa walimu katika ufundishaji na ujifunzaji darasani.

Katika kuongeza ufanisi wa ufundishaji na ujifunzaji darasani, Taasisi ya Elimu Tanzania kwa kushirikiana na EQUIP-Tanzania, wameandaa moduli hii ambayo imesheheni kazi mbalimbali ambazo waalimu mtazitenda katika vikundi wakati wa mafunzo kwa kutumia mbinu ya Mafunzo ya Walimu Kazini ngazi ya shule. Mbinu hii inatambua umuhimu wa walimu kujifunza pamoja na kubaini changamoto zinazowakabili ili kupata suluhisho la changamoto za ufundishaji na ujifunzaji kwa pamoja.

Moduli hii ya Mafunzo ya Walimu Kazini, imeandaliwa ili kusaidia juhudi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuhakikisha kuwa mbinu fanisi zinatumika darasani wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Moduli hii pia inawasaidia walimu kushirikishana uzoefu na umahiri katika ufundishaji na ujifunzaji darasani. Vilevile Moduli inatoa mafunzo ya ziada ikitarajiwa kuwa walimu watakuwa wamekwisha pata Mafunzo Kabilishi ya utekelezaji wa Mtaala ulioboreshwa wa kuimarisha ufundishaji wa KKK kwa wanafunzi wa darasa la kwanza na la pili.

Taasisi ya Elimu Tanzania inatarajia kuwa moduli hii itawasaidia walimu kuimarisha umahiri wa ufundishaji na ujifunzaji ili kuwasaidia wanafunzi waweze kujenga uwezo unaokusudiwa wakati wa kujifunza.

Changamoto iliyo mbele yetu ni kuhakikisha kuwa tunaonyesha kwa vitendo matokeo mazuri yanayotokana na maudhui ya moduli hii wakati wa ufundishaji na ujifunzaji darasani ili kuimarisha ubora wa elimu ya shule ya msingi.

Dr. Leonard Akwilapo
Kaimu Mkurugenzi Mkuu,
Taasisi ya Elimu Tanzania.

Maelezo Muhimu kwa Mratibu wa Mafunzo ya Walimu Kazini Ngazi ya Shule

Mwongozo huu utatumika sanjari na moduli ya nane ya mwalimu ili kumsaidia mratibu wa mafunzo kuwa na mpangilio mzuri wenye kufuata hatua kwa hatua ili kuwafanya walimu washiriki kikamilifu katika kujifunza maudhui ya moduli ya nane.

Mwongozo huu umegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ambayo ni upande wa kushoto wa mwongozo unabeba maelezo ambayo mratibu wa mafunzo ya walimu kazini ngazi ya shule atatakiwa kuyafuata wakati wa kuratibu kipindi cha kujifunza maudhui ya moduli. Sehemu ya pili ambayo ni upande wa kulia wa mwongozo unabeba maudhui yaliyo kwenye moduli ya mwalimu ambayo watayasoma wakati wa kipindi cha kujifunza.

Wakati wa kipindi cha kujifunza, unatakiwa kufuata maelezo yanayokuongoza yaliyo upande wa kushoto wa mwongozo huu na kuyahusianisha na maudhui yaliyo kwenye moduli ya mwalimu ambayo yapo upande wa kulia wa mwongozo huu kama yanavyosomeka kwenye moduli ya mwalimu.

MAELEKEZO NA TASWIRA KATIKA MODULI

Kuna picha na michoro mingi katika moduli. Baadhi zinajirudia mara nyingi kwa sababu zinamaanisha jambo mahususi linalotokea. Zifuatazo ni mifano ya taswira mbalimbali ambazo zinapatikana katika moduli pamoja na kile ambacho zinawakilisha:

Jadili na mwenzako: Wakati wote wa kusoma moduli, walimu wataelezwa kufanya kazi pamoja na mwalimu mwingine juu ya maswali au kazi.

Fikiri – Wawili wawili – Shirikishana: Kama ilivyo katika maelezo ya hapo juu, hapa vilevile walimu wanafanya kazi wakiwa wawili wawili. Japokuwa, hapa walimu wanatafakari mmoja mmoja kwanza juu ya swali au tatizo, halafu mwalimu anafanya kazi na mwenzake na mwishoni wanawasilisha katika kundi lote.

Jadiliana katika kikundi: Wakati mwingine walimu wataelekezwa kutafakari au kujadili maswali mbalimbali katika kikundi.

Soma: Katika kila moduli kuna "dhana kuu" ambayo kwa kawaida huwasilishwa kwa kirefu katika maelezo.

Andika: Moduli itawahamasisha walimu kuchukua maelezo na kuandika fikra zao na majibu.

Igizo: Baadhi ya mazoezi yatahitaji walimu kuigiza kazi ya kufundisha wakati wengine watapaswa kuigiza kama wanafunzi.

MAELEKEZO KWA MRATIBU WA MAFUNZO YA WALIMU KAZINI

Kabla ya kuanza moduli hii, angalia 'maelekezo muhimu' na hakikisha kuwa wewe na walimu mnayazingatia.

Tafadhali waambie walimu wajiorodheshe na kusaini hapa chini.

WAAMBIE WALIMU:

"Sasa tutasoma utangulizi wa moduli hii. Tutasoma kwa sauti matini kwa kupokezana. Baada ya mwalimu wa kwanza kusoma aya ya kwanza, atamwita mwalimu mwingine kwa jina ili asome aya inayofuata."

Tarehe:	Shule:	Wilaya:	Mkoa:
Muda wa kuanza:	Jina la Mratibu na sahihi yake:		
Muda wa kumaliza:	Jina la Mwalimu Mkuu na sahihi yake:		

	JINA LA MWALIMU	ME / KE	SAHIHI:	DARASA
1				
2				
3				
4				
5				
6				
7				
8				

MODULI YA 8: FONIKI

MAUDHUI YA MODULI

Kipindi hiki kinahusu **foniki**, ambayo ni mchakato wa kuoanisha sauti za herufi kwa alama zilizoandikwa ambazo zinaziwakilisha. Foniki ni mbinu kuu katika kujifunza namna ya kusoma, kwa sababu inageuza alama zilizoko kwenye ukurasa kuwa maneno yanayotamkwa na ambayo yanabeba maana.

DHANA KUU

- **Kuachanisha sauti** – kutenganisha sauti kutoka kwa nyingine katika kila neno (/m/ /t/ /i/ = mti)
- **Sauti ya herufi** – sehemu ndogo ya sauti ambayo inatengenezwa na herufi katika neno linalotamkwa. Sauti za herufi zinaandikwa ndani ya mistari mshazari kama hivi / / (kwa mfano, sauti ya herufi 'm' inaandikwa /m/)
- **Jina la herufi** – ni namna ya kurejea kwenye herufi (kama unavyotamka alfabeti au kutamka neno). Majina ya herufi siyo sawasawa na sauti za herufi. Kama unaandika jina la herufi tumia funga na fungua semi : 'm '

MALENGO YA MODULI

Mwisho wa kipindi hiki, mwalimu atakuwa na uwezo wa:

- Kuelewa namna gani uhusiano wa sauti na herufi unasaidia katika usomaji
- Kutathmini uwezo wa wanafunzi katika foniki.
- Kutumia njia na mbinu mbalimbali ili kuimarisha ujuzi wa wanafunzi katika foniki
- Kutengeneza bango la alfabeti ili kukuza mbinu za kusaidia kufundisha foniki

---

MAELEKEZO MUHIMU

1. Mara zote njoo na moduli ya mafunzo ya walimu kazini na kalamu
2. Unaweza kuja na chakula au kitu cha kutafuna na maji kama mtapanga kukutana mchana baada ya masomo
3. Njoo na kadi picha ulizotengeneza katika kipindi kilichopita
4. Chaki
5. Rula 2 au vijiti 2
6. Vipande 24 vya karatasi za A4 kwa kila mwalimu (jaribu kuwa na vipande 19 katika rangi moja, na vipande 5 katika rangi nyingine kama inawezekana)
7. Mkasi
8. Viweka alama
9. Kamba

TARATIBU ZA KUJIFUNZA KWA KILA KIPINDI

- Kutana katika sehemu tulivu yenye ubao kama inavyoonekana katika picha
- Panga madawati/meza ili kuwezesha washiriki wote waonane na kuongea kwa pamoja
- Kuwa huru kuuliza maswali kama hujaelewa
- Kuwa wa msaada kwa wenzako
- Kuwa mbunifu na fikiria namna dhana unazojifunza zinahusiana na darasa lako
- Weka simu yako katika hali ya mtetemo

TAFAKARI

WAAMBIE WALIMU:

“Tangu moduli ya 7, umefanyia mazoezi shughuli mbili kwenye kipindi cha kujifunza kusoma na kuandika. Orodhesha mafanikio uliyoyaona pamoja na changamoto ulizokabiliana nazo wakati wa kufundisha maudhui ya moduli hiyo darasani kwako

Una dakika 5 kwa ajili ya kazi hii.”

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa tutajadiliana kwa pamoja, mafanikio na changamoto katika kikundi.

Kwa kila changamoto ambayo imewasilishwa tufikiri kwa pamoja kuhusu namna ya kukabiliana nayo. Kumbuka kuandika ufumbuzi ambao unaweza kukabiliana na changamoto zilizojitokeza. Tutatumia dakika 10 kwa majadiliano.”

TAFAKARI

Katika kipindi kilichopita tulisoma utambuzi wa sauti. Orodhesha mafanikio uliyoyaona pamoja na changamoto ulizokabiliana nazo wakati wa kufundisha maudhui ya moduli hiyo darasani kwako.

ANDIKA PEKE YAKO (DAKIKA 5)
Tafadhali andika kwenye visanduku mafanikio na changamoto ulizokutana nazo wakati wa kutekeleza mikakati hiyo katika darasa lako.

Mafanikio
(Elezea utaratibu uliotumia na fafanua namna ulivyofanikiwa)

Changamoto
(Elezea utaratibu uliotumia na fafanua changamoto zake)

JADILIANA KATIKA KIKUNDI (DAKIKA 10)
- Shirikisha wenzako kwenye kundi kuhusu mojawapo ya uzoefu huo.
- Kwa kila changamoto, pendekeza namna ya kukabiliana nayo.
- Wakati wa majadiliano, andika ufumbuzi unaoendana na changamoto ulizobainisha.

Njia Muhimu za Ufumbuzi
(Mawazo muhimu na mahsusi kwa wenzetu)

UTANGULIZI

(Kabla ya kipindi, andika herufi kwenye ubao kama hapa chini.)





WAAMBIE WALIMU:

"Sasa tuanze kusoma maelekezo kwa ajili ya zoezi la kuchangamsha mwili."

Walimu wanapomaliza kusoma na wako tayari kucheza, sema sauti za herufi ambazo zimeorodheshwa hapa. Tulia kila baada ya sauti ya herufi moja ili walimu waweze kushindana kuonesha herufi sahihi. Kama wako sahihi, waruhusu waseme neno kwa sauti ya herufi hiyo. Kama hawako sahihi, ruhusu mwalimu mwingine aoneshe herufi sahihi na aseme neno sahihi.

1)	/t/	2)	/j/
3)	/w/	4)	/v/
5)	/l/	6)	/r/
7)	/s/	8)	/z/
9)	/n/	10)	/i/
11)	/a/	12)	/m/
13)	/p/	14)	/f/
15)	/o/	16)	/e/

WAAMBIE WALIMU:

"Kwa kuwa sasa tumemaliza, tafadhali soma maswali peke yako na fikiria utakavyoyajibu. Jadili majibu yako na mwenzako. Kisha utashirikisha mawazo yako kwenye kikundi."

Baada ya dakika 2, wajulishe walimu wabadilishane mawazo kuhusu majibu yao. Hapa kuna baadhi ya majibu:

Jibu la 1: sauti ya herufi
Jibu la 2: herufi zilizo andikwa
Jibu la 3: Kama wanafunzi wataweza kuhusianisha sauti na herufi zilizoandikwa, watakuwa na uwezo wa kutamka neno lililoandikwa kwa kutengeneza sauti inayoundwa na kila herufi kwenye neno

UTANGULIZI

ZOEZI LA KUCHANGAMSHA (DAKIKA 10)

Zoezi la kuchangamsha la leo linahitaji tuelekeze akili zetu kwenye sauti za herufi, am bazo ni sauti zinazotengenezwa wakati zinatamkwa katika maneno. Kumbuka kwamba sauti ya herufi ni tofauti na jina la herufi. Kwa mfano, sauti ya herufi /m/ ni sauti ambayo unaitengeneza unaposema 'mtu' au 'mti'. Jina la herufi ya sauti 'm' linasikika kama silabi 'me'.

Sasa, haya ndiyo maelekezo ya mchezo.

1. Mratibu wa mafunzo ya walimu kazini aandike herufi mbalimbali tofauti kwenye ubao. Mratibu wa mafunzo ya walimu kazini atatamka sauti ya moja ya herufi zilizoko ubaoni.

2. Walimu wawili watajitolea kuja kwenye ubao wakiwa na rula ndefu.

3. Walimu wawili watashindana kuonesha herufi iliyotamkwa na mratibu na kuitaja. Mwalimu ambaye atawahi kuonesha herufi na kutaja neno atapata alama.

4. Ikiwa mwalimu ataonesha herufi zisizo sahihi au ambazo hazitengenezi neno sahihi, mwalimu mwingine atakuwa na nafasi kuonesha herufi sahihi na kutamka neno kwa usahihi. Kama ziko sahihi, zinabakia na mwalimu mwingine lazima awe amekaa chini.

5. Wakati Mwalimu atakayekuwa amepata alama nyingi atakuwa ameshinda.

6. Mratibu ataita jozi zingine na kuendelea hadi herufi zote zimalizike .



FIKIRI - WAWILI WAWILI - SHIRIKISHANA (DAKIKA 5)

Ukishamaliza kucheza mchezo huu, jadili maswali yafuatayo ukiwa na mshirika wako:

1. Wakati wa mchezo huu ulikuwa unasikiliza nini?
2. Wakati wa mchezo huu ulikuwa unaangalia nini?
3. Kwa nini ni muhimu kuhusianisha sauti za herufi na herufi zilizoandikwa?

DHANA KUU

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa tutasoma maudhui muhimu. Tutasoma matini kwa sauti na kwa kupokezana.

Baada ya mwalimu wa kwanza kusoma sehemu (kwa mfano, aya au maelezo), atamwita mwalimu mwingine kwa jina ili asome sehemu inayofuata.

Wakati wa kusoma weka alama zifuatazo kwenye matini unayosoma.

Weka alama ya mshangao (!) kwenye wazo ambalo unadhani ni muhimu.

Weka alama ya kuuliza (?) kuonesha kutokukubaliana na dhana hiyo.

Weka alama ya duara (o) kuonesha kuwa dhana hiyo ni mpya kwako.”

DHANA KUU

UMUHIMU WA FONIKI (DAKIKA 25)

1. Mwalimu mmoja aanze kusoma kwa sauti. Baada ya kukamilisha sehemu (kwa mfano, aya au maelezo) amwite mwalimu mwingine kwa jina asome sehemu inayofuata.
2. Wakati unaposoma zingatia alama zifuatazo:
   - Weka alama ya mshangao (!) katika sehemu ambayo unaona ni muhimu
   - Weka alama ya kuuliza (?) katika sehemu ambayo huelewi au hukubaliani nayo
   - Weka mduara katika (o) maneno ambayo ni mapya.

Kama utakumbuka kutoka kwenye moduli ya 7, tulijadili namna wanafunzi wengi wanavyoanza shule wakifahamu Kiswahili kinachoongewa tu (au lugha zao za kwanza). Ili wanafunzi waweze kusoma na kuandika Kiswahili, wanapaswa kuelewa kwamba:

Leo, moduli hii inajikita katika hatua ya 2, kuwasaidia wanafunzi kuelewa kwamba sauti zinazotengeneza maneno zinahusiana na herufi. Dhana hii inaitwa foniki. Foniki ni mchakato wa **kuhusianisha sauti za herufi kwenye herufi zilizoandikwa ambazo zinaziwakilisha.**

Zoezi la kuchangamsha mwili lilikuwa mfano wa **utambuzi wa sauti za herufi** (ambazo ulijifunza katika moduli ya 7) na **foniki.** Ulitumia ujuzi wako wa utambuzi wa sauti za herufi wakati ulipomsikiliza mratibu wa mafunzo ya walimu kazini, kutamka sauti za herufi, na ulitumia ujuzi wako wa **foniki** wakati ulipohusianisha sauti kwenye herufi ziliyoandikwa.

<u>Kujua sauti ya herufi inayoambatana na kila herufi iliyoandikwa ndiyo ujuzi mkuu katika foniki.</u>

Kumbuka, sauti ya herufi ni tofauti na jina la herufi. Sauti ya herufi ni sauti ambayo unaitengeneza wakati unatamka herufi katika neno linalotamkwa. Ni rahisi kutambua sauti za herufi wakati unatamka neno taratibu na kuwa makini namna midomo yako na ulimi vinavyobadilika wakati unatamka kila herufi. Kwa mfano, ukiwa unatamka neno 'nje' taratibu sana, unaweza kusikia kirahisi sauti ya herufi ya kwanza, ambayo ni tofauti kutoka kwenye jina la herufi. Tamka taratibu: /nnn/ /jjj/ /eee/

Kumbuka pia, sauti za herufi ndefu ni nyepesi kutambua na kutamka kuliko sauti za herufi fupi kwa sababu unaweza kuzivuta kwa sekunde kadhaa, kama /m/, /n/, /s/, /z/ na irabu nyingine.

DHANA KUU

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa tunaweza kushiriki katika utambuaji wa sauti za herufi tukiwa na mshirika. Halafu tutaendelea kusoma baada ya kumaliza.”

(Baada ya walimu kumaliza, waulize kama wana matatizo yoyote katika kutambua sauti za herufi)

“Sasa tuendelee kusoma”

DHANA KUU

Jambo lingine la kukumbuka kuhusu sauti za herufi ni namna unavyorejea katika mfumo wa uandishi. Japokuwa umeona /nnn/ /jjj/ /eee/, hii ilifanyika kusisitiza kwamba ni lazima useme sauti za herufi polepole sana. Japokuwa, katika hali halisi kuna herufi moja tu iliyoandikwa kati ya mistari mshazari miwili:/n/. Hii ni tofauti na unavyoandika jina la herufi, ambayo ni herufi moja iliyoandikwa kati ya alama mbili za nukuu : 'n'.

Jina la herufi ni kanuni inayotambulika katika kuitambua herufi ya jina katika lugha husika. Kwa mfano, jina la herufi 'n' linasikika kama silabi 'ne', ambayo ni tofauti kuliko sauti ya herufi ambayo inatengenezwa wakati unasema 'nje' au 'ndoo'.

Kumbuka kwamba majina ya herufi za Kiswahili yana tofauti na yale ya Kiingereza. Majina ya herufi za Kiswahili lazima yatamkwe kama:
a, be, che, de, e, fe, ge, he, i, je, ke, le, me, ne, o, pe, re, se, te, u, ve, we, ye, ze

Ili kuendelea kushiriki kutambua sauti za herufi kwa ajili ya herufi mahsusi ziliyoandikwa, angalia katika mfano hapa chini. Ili kutambua sauti za herufi kwa ajili ya herufi iliyoandikwa 'z', sikiliza sauti zinazofahamika baina ya silabi.

Tamka taratibu sana: **za ze zi zo zu**

/zzz/ /aaa/ /zzz/ /eee/ /zzz/ /iiii/ /zzz/ /ooo/ /zzz/ /uuu/

Ni sauti zipi zinazofahamika umezisikia? Sauti inayofahamika ni sauti ya herufi 'z'. Unaweza pia kusema kwa sababu uliziba meno yako kusema sauti /zzz/ na tena meno yako yafunguliwe kusema irabu tofauti.

Sasa, fanya pamoja na mshirika:

1. **Herufi 'f' inaunda sauti gani?** (Kama umekwama, fikiria kuhusu sauti zinazofahamika kwenye: /fa/ /fe/ /fi/ /fo/ /fu/)
2. **Herufi 'p' inaunda sauti gani?** (Kama umekwama, fikiria kuhusu sauti zinazofahamika kwenye: /pa/ /pe/ /pi/ /po/ /pu/)
3. **Herufi 'k' inaunda sauti gani?** (Kama umekwama, fikiria kuhusu sauti zinazofahamika kwenye: /ka/ /ke/ /ki/ /ko/ /ku/)
4. **Herufi 'w' inaunda sauti gani?** (Kama umekwama, fikiria kuhusu sauti zinazofahamika kwenye: /wa/ /we/ /wi/ /wo/ /wu/)

Mbinu za Kufundisha foniki

Katika moduli ya 7 tulijadili mbinu za kuwasaidia wanafunzi kuachanisha sauti tofauti katika maneno yanayotamkwa (kupitia mbinu kama Binya Vidole). Mara tu wanafunzi wanapozifahamu sauti hizi zilizoachana, unaweza kuwaonesha sauti zinazohusiana na herufi hizi. Kwa mfano:

1. Wanafunzi wafanye zoezi la Binya Vidole kwa maneno ambayo yanaanza na mwanzo wa sauti unaofanana. Kwa mfano, mama, mimi, meza, muda, mwisho. Hii inasaidia wanafunzi kusikia sauti /m/ katika muktadha tofauti.
2. Waambie watambue sauti ya mwanzo ya maneno haya. Lazima watamke /mmm/.

DHANA KUU

DHANA KUU

3. Halafu andika au onesha kwenye herufi 'm' na eleza kwamba hii ni herufi ambayo inatengeneza sauti hiyo. Wanafunzi wa darasa la 2 na la 3 watakuwa wameshafahamu herufi za alfabeti. Hii ni sawa, hakikisha wanafahamu kwamba jina la herufi 'm' ni tofauti kuliko sauti inayotengenezwa.
4. Andika maneno mama, mimi, meza, muda, mwisho, kwenye ubao na onesha namna herufi 'm' inavyotengeneza maneno yote kwa kuanza na sauti /mmm/.

Unaweza kutumia mbinu pamoja na orodha ambayo huwa unaitumia kufundishia herufi za alfabeti. Japokuwa, pia unaweza kuwa unafikiri kuhusu kubadilisha orodha ili kwanza uanze na sauti za maneno/herufi zinazofahamika zaidi. Wanafunzi watakuwa na uelewa mkubwa na sauti hizi na wataona herufi mara nyingi zaidi. Hii inamaanisha kuwa watajifunza sauti za herufi haraka. Baadhi ya herufi zinazofahamika zaidi katika Kiswahili ni 'm', 'n', 's', b', 'd', 'k' na irabu. Baada ya kuanza na herufi hizi, pitia alfabeti zote zilizobakia, tena jaribu kujielekeza kwanza kwenye sauti za herufi zinazofahamika zaidi. Moduli yote iliyobakia italeta mbinu mbalimbali tofauti za kufundisha foniki.

Kwa nini ujuzi wa foniki ni muhimu?

Ngoja tuangalie mfano wa namna ya kutumia sauti za herufi kusoma. Hapa chini kuna maneno ambayo unaweza kuwa hauyajui. Kila mwalimu lazima achukue jukumu la kusoma neno tofauti kwa sauti, kwa kutumia ujuzi wake wa sauti za herufi.

1. Ichi	**2. Ni**	**3. San**	**4. Shi**	**5. Go**	**6. Roku**	**7. Shichi**	**8. Hachi**	**9. Ku**	**10. Juu**

Unajua nini? Umeshahesabu hadi 10 kwa Kijapani. Bila kuijua lugha, umekuwa na uwezo wa kutumia maarifa yako ya sauti herufi kutamka maneno haya kwa usahihi. Huu ni mchakato uleule kwa ajili ya watoto wadogo wanaojifunza kusoma Kiswahili kwa mara ya kwanza. Kama wanafunzi wataweza kuhusianisha sauti na herufi zilizoandikwa, watakuwa na uwezo wa kutamka neno lililoandikwa kwa kutengeneza sauti inayoundwa na kila herufi kwenye neno. Hii inamaanisha watakuwa na uwezo wa kusoma kwa sauti maneno yasiyofahamika, hata kama bado hawajui yanachomaanisha.

DHANA KUU

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa kila mwalimu anaweza kushirikisha walimu wengine kitu ambacho ameona ni muhimu, hakieleweki au ni kipya. Halafu tunaweza kujadili kwa nini ni muhimu kwa wanafunzi kuwa na uwezo wa kuhusianisha sauti za herufi na herufi zilizoandikwa.”

Elekeza kila mwalimu kubadilisha mawazo na wenzake juu ya majibu yake. Kama walimu wana matatizo na swali la nne, hapa chini kuna majibu ya kuwapatia:

Jibu la 4: Kama wanafunzi wanajua sauti za herufi, watakuwa na uwezo wa kutamka neno lililoandikwa kwa kutengeneza sauti ya kila herufi kwenye neno. Hii inamaanisha wanaweza kusoma kwa sauti maneno wasiyoyajua, hata kama hawajui yanamaanisha nini.

DHANA KUU

JADILIANA KATIKA KUNDI KUBWA (DAKIKA 10)

1. Ni dhana ipi muhimu uliyoweka alama ya mshangao (!)?
2. Ni dhana ipi ambayo haieleweki uliyoiwekea alama ya kuuliza (?)?
3. Ni dhana ipi mpya uliyoizungushia duara?
4. Kwa nini ni muhimu kwa wanafunzi kuwa na uwezo wa kuoanisha sauti za herufi kwa herufi zilizoandikwa?

ZOEZI

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa tutaanza kusoma sehemu inayofuata kwa sauti. Baada ya mwalimu wa kwanza kukamilisha aya, anaweza kuita jina la mwalimu mwingine ili aendelee kusoma aya inayofuata.”

ZOEZI

MBINU ZA KUFUNDISHA FONIKI (DAKIKA 20)

Njia nyingine ambayo tunaweza kuitumia kuwasaidia wanafunzi kuhusianisha sauti na herufi ni kwa kutumia mbinu ya **jina-neno kuu-sauti.** Mbinu hii inataka mwanafunzi abainishe na kukumbuka:

1. Jina la herufi
2. Neno kuu kusaidia kukumbuka sauti ya herufi
3. Sauti iliyoachanishwa iliyoambatanishwa na herufi hiyo

Mbinu hii inawasaidia wanafunzi kuhusianisha jina la herufi na sauti i. Mwanafunzi anaposema neno kuu, anasema pia sauti ya herufi na hii inawasaidia kuikumbuka. Mara tu wanafunzi wanapokumbuka sauti za herufi zote zilizoandikwa, watakuwa na uwezo wa kutamka neno lililoandikwa kwa kutengeneza sauti za kila herufi kwenye neno. Hii inamaanisha wanaweza kusoma kwa sauti maneno wasiyoyafahamu, hata kama hawajui maana yake.

Ni muhimu kuanza kufundisha kwanza herufi zinazofahamika zaidi, ili wanafunzi waweze kujifunza kusoma maneno na sentensi ifikapo mwisho wa wiki za mwanzoni mwa mafunzo.

1. Herufi zinazofahamika sana ni: m, n, s, b, d, k na irabu a, e, i, o, u
2. Herufi zinazofuatia kwa kufahamika ni: t, p, ch, l, f, j
3. Kundi la mwisho la herufi ni: g,y, z, h, r, w, v

Tumia mbinu ya **jina-neno kuu-sauti** wakati unafundisha kila herufi. Wakati unafundisha mbinu ya **jina-neno kuu-sauti** kwa wanafunzi, unapaswa mara zote kuifanya kwa namna ileile kwa kutumia maneno makuu yaleyale. Kwa mfano, rejea hatua zifuatazo: Katika hatua hizi tumia mbinu ya 'Nina fanya - Tunafanya - Mnafanya'. Anza kwa kuonesha mfano, kisha fanya pamoja na wanafunzi na mwisho waambie wanafunzi wafanye wenyewe.

Hatua ya 1: Onesha herufi iliyoandikwa kwenye kadi au ubaona tamka **jina la herufi**. Wanafunzi wanaweza kurudia baada yako.



Hatua ya 2: Halafu shikilia kadi picha inayohusiana na herufi hiyo. Sema **neno kuu** na watake wanafunzi warudie baada yako. (Kwa kusema neno kuu, wanafunzi wanasema sauti ya herufi moja kwa moja.

Hatua ya 3: Imarisha **sauti ya herufi** kwa kutamka sauti ya herufi ikiwa yenyewe. Onesha kwenye midomo yako wakati unasema.

ZOEZI

WAAMBIE WALIMU:

"Sasa, ngoja tushiriki mbinu ya jina-neno kuu – sauti"

Chagua mtu ambaye ataanza kushiriki katika zoezi.
Andika herufi zifuatazo – moja kwa kila mtu kwenye kundi ('n' 's' 'f' 'm' ' r')

Halafu kwenye ubao, andika Jina kuu na sauti ambayo mwalimu ametoa.



WAAMBIE WALIMU:

"Tafadhali soma maswali peke yako na kisha fikiria majibu yako. Jadili majibu yako na mwenzako. Kisha shirikisha mawazo yako katika kikundi."

Wapatie walimu dakika 5 kujadili, halafu waelekeze wabadilishane mawazo kuhusu majibu. Kama walimu watakwama, hapa kuna baadhi ya majibu:

Jibu la 1: Mbinu hii inawasaidia wanafunzi kuunganisha majina ya herufi kupitia kwenye neno kuu. Mwanafunzi anaposema neno kuu, anasema sauti ya herufi na hii inamsaidia kukumbuka.

Jibu la 2: Kama wanafunzi wanajua sauti za herufi zilizoandikwa, watakuwa na uwezo wa kutamka neno lililoandikwa kwa kutengeneza sauti kwa kila herufi katika neno hata kama haifahamiki.

Jibu la 3: Kila unapofundisha herufi mpya kwa darasa, fundisha kwa kutumia mbinu ya jina – neno kuu – sauti.

ZOEZI

Sasa, ngoja tushiriki mbinu ya <u>jina – neno kuu – sauti:</u>

1. Kundi lote linaweza kushiriki pamoja. Mratibu wa Mafunzo ya Walimu Kazini atachagua mtu mmoja kuanza.
2. Mratibu ataandika herufi kwenye ubao.
3. Mtu wa kwanza atapaswa kwanza kusema: **jina la herufi**
4. Halafu wanapaswa kusema: **neno kuu** (kitu kinachofahamika ambacho kinaanza na herufi hiyo)
5. Kama ukishakuwa na kadi za picha zako tayari, unaweza kushikilia picha ya neno kuu.
6. Halafu mtu huyo anapaswa kutamka: **sauti ya herufi**
7. Baada ya mtu wa kwanza kusema **jina – neno kuu – sauti,** kundi zima lililobakia litarudia.
8. Halafu mtu anayefuatia anaendelea na zoezi hili (Hatua ya 3 – 6) hadi kila mmoja katika kundi anakuwa ameongoza mfuatano wa **jina – neno kuu** – sauti walau mara moja.

FIKIRI - WAWILI WAWILI - SHIRIKISHANA (DAKIKA 10)

Ukishamaliza kushiriki jina – neno kuu – sauti, jadili maswali haya na mshirika na halafu katika kundi:

1. Namna gani mkakati huu unawasaidia wanafunzi kuhusianisha majina ya herufi na sauti?
2. Namna gani ukumbukaji wa sauti za herufi unawasaidia wanafunzi kusoma maneno wasiyoyafahamu?
3. Ni wakati gani unaweza kutumia mbinu ya jina – neno kuu – sauti katika kufundisha kusoma katika darasa lako?

KUPANGA MKAKATI

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa tutasoma kuhusu kuandaa kipindi cha kusoma na kuandika. Tutasoma matini kwa sauti na kwa kupokezana.

Baada ya mwalimu wa kwanza kusoma sehemu (kwa mfano, aya au maelezo), atamwita mwalimu mwingine kwa jina ili asome aya inayofuata. “

KUPANGA MKAKATI

KUANDAA 'KIPINDI CHA KUSOMA NA KUANDIKA' (DAKIKA 30)
Katika kuimarisha umahiri wa wanafunzi kujifunza kusoma na kuandika, ni muhimu mwalimu awe na mpango unaomwezesha kutumia maarifa mapya aliyojifunza wakati wa mafunzo ya walimu kazini kwa vitendo. Aidha, ni muhimu kwa wanafunzi kupata muda zaidi wa kujifunza kusoma na kuandika.

Kurasa zifuatazo zimesheheni mifano ya somo kazi wa jumla kwa ajili ya kazi mbili ambazo pamoja na mshirika mwingine unaweza kujaribu wakati wa vipindi vya kusoma na kuandika (au unaweza kujaribu wakati wa kipindi cha kawaida cha Kiswahili).

1. Soma kila mwongozo wa somo
2. Jaza nafasi zilizo wazi katika kila mwongozo wa somo
3. Halafu jaribu mikakati wakati wa kipindi cha kusoma na kuandika.

MWONGOZO WA SOMO NAMBA 1: Jina – Neno kuu - Sauti

UMAHIRI MKUU: Ufahamu wa sauti na jina la herufi

LENGO KUU: Mwanafunzi aelewe majina ya herufi na sauti zao

LENGO MAHSUSI: Mwanafunzi aweze kubaini sauti na jina la herufi kwa kutumia mbinu ya 'Jina-Neno kuu-Sauti'

UMAHIRI MAHSUSI: Kubainisha jina la herufi na sauti ya herufi

ZANA ZA KUFUNDISHA: Kadi za picha

VITABU VYA REJEA: Moduli ya 8

MCHAKATO WA UFUNDISHAJI

HATUA	MUDA	VITENDO VYA UFUNDISHAJI	VITENDO VYA KUJIFUNZA
UTANGULIZI	**5**	1. Anza kipindi na wimbo, kama 'Wimbo ya Alfabeti' ambao ulijadiliwa katika moduli ya 1. 2. Kumbuka kwamba majina ya herufi za Kiswahili ni tofauti sana na majina ya herufi za Kiingereza. Majina ya herufi za Kiswahili yanasikika kama silabi zinazoongezewa 'e' kwenye konsonanti. Kwa mfano: be, che, de, fe. Japokuwa, majina ya herufi kwa ajili ya irabu ni sawa na sauti za herufi zake : a, e, i, o, u.	

KUPANGA MKAKATI

(Zunguka uangalie kama walimu wanahitaji msaada)

KUPANGA MKAKATI

HATUA	MUDA	VITENDO VYA UFUNDISHAJI	VITENDO VYA KUJIFUNZA
MAARIFA MAPYA	**5**	3. Chagua herufi ambayo utaiwekea mkazo katika somo. Unaweza kuanza na herufi inayofahamika zaidi kwanza: m, n, s, b, d, k na irabu a, e, i, o, u. 4. Herufi zinazofuatia kwa kufahamika ni : t, p, ch, l, f, j 5. Kundi la mwisho la herufi ni: g,y, z, h, r, w, v 6. Waambie wanafunzi kwamba tutakuwa tunajifunza mchezo uitwao 'Jina – Neno kuu - Sauti'. Unaweza kutumia mbinu ya 'Ninafanya – Tunafanya – Mnafanya' kufudisha mchezo huu. 7. Kwanza, anza na 'Ninafanya': Onesha herufi iliyoandikwa kwenye kadi au ubao na tamka jina la herufi. Kwa mfano, 'n' (kumbuka unatamka 'ne'). 8. Kisha, endelea na 'Tunafanya': Himiza wanafunzi watamke 'n' pamoja na wewe. 9. Mwisho, maliza na 'Mnafanya': Himiza wanafunzi watamke 'n' wenyewe. 10. Halafu shikilia kadi picha inayohusiana na herufi hiyo. Anza na 'Ninafanya': Tamka neno kuu kama 'nazi'. Endelea na 'Tutafanya': Himiza wanafunzi watamke 'nazi' pamoja na wewe. Maliza na 'Mnafanya': Himiza wanafunzi watamke 'nazi' wenyewe. (Kwa kusema neno kuu, wanafunzi wanasema sauti ya herufi moja kwa moja). 11. Imarisha sauti ya herufi kwa kutamka sauti ya herufi ikiwa yenyewe. Anza na 'Ninafanya': Tamka sauti ya herufi /n/ (onesha kwenye midomo yako wakati unasema). Endelea na 'Tutafanya': Himiza wanafunzi watamke /n/ pamoja na wewe. Maliza na 'Mnafanya': Himiza wanafunzi watamke /n/ wenyewe.	**Sikiliza maelezo ya walimu kuhusu Jina – neno kuu - sauti**
KUIMARISHA MAARIFA	**10**	12. Mara baada ya wanafunzi wengi kuweza kutamka kwa usahihi Jina – Neno kuu – Sauti wao wenyewe, rudia orodha kinyumenyume na anza na sauti ya herufi. Waambie wanafunzi kuwa neno kuu linaanza na sauti ya herufi hiyo, halafu wafanye wanafunzi waseme jina la herufi. 13. Kama una muda, unaweza pia kuwauliza wanafunzi kufikiria maneno makuu mengine ambayo yanaanza na jina la herufi na sauti ya herufi ambayo unayatumia.	**Muige mwalimu katika kutumia mbinu ya Jina – neno kuu – sauti.**

KUPANGA MKAKATI

(Zunguka uangalie kama walimu wanahitaji msaada)

KUPANGA MKAKATI

HATUA	MUDA	VITENDO VYA UFUNDISHAJI	VITENDO VYA KUJIFUNZA
KUTUMIA MAARIFA	**15**	14. Wafanye wanafunzi wafanye zoezi hili wakiwa wawiliwawili. Kwanza waanze kufanyia mazoezi jina – neno kuu – sauti. Halafu, waambie wajaribu sauti – neno kuu – jina. Mwisho, waambie wajaribu jina – neno kuu – sauti 15. Wakati wanafunzi wanashiriki wakiwa wawili wawili, anzisha kundi dogo la wanaojifunza polepole. Pitia hatua ya 5 – 7 taratibu pamoja nao hadi waelewe.	**Shiriki mbinu hii mkiwa wawiliwawili.**
UPIMAJI	**10**	16. Fanya mazoezi ya mdomo unapoonesha kadi picha na waulize wanafunzi kwanza watamke sauti ya herufi. 17. Uliza wanafunzi waoneshe herufi iliyoandikwa au waiandike kwenye ubao. 18. Unaweza kufanya hivi na herufi zingine ambazo umekwishazifundisha. 19. Kama unaona kuna wanafunzi hawaelewi, rudia kufundisha herufi.	**Wanafunzi wanaweza kukumbuka sauti na jina kwa herufi zilizoandikwa.**

Tathmini: _____

Maoni: _____

MWONGOZO WA SOMO NAMBA 2: Onesha herufi

UMAHIRI MKUU: Kubainisha jina la herufi na sauti zao za herufi

LENGO KUU: Mwanafunzi aelewe majina ya herufi na sauti zao

LENGO MAHSUSI: Mwanafunzi aweze kubaini jina la herufi na sauti ya herufi kwa kutumia mbinu ya 'Onesha herufi'

UMAHIRI MAHSUSI: Kuunganisha majina ya herufi kwenye sauti zao za herufi

ZANA ZA KUFUNDISHA: Orodha ya herufi na rula 2 (au vijiti 2)

VITABU VYA REJEA: Moduli ya 8

KUPANGA MKAKATI

(Zunguka uangalie kama walimu wanahitaji msaada)

KUPANGA MKAKATI

MCHAKATO WA UFUNDISHAJI

HATUA	MUDA	VITENDO VYA UFUNDISHAJI	VITENDO VYA KUJIFUNZA
UTANGULIZI	**5**	1. Mchezo huu unaweza kutumika baada ya kuwa umefundisha walau herufi 4. 2. Njoo na rula mbili katika kipindi. 3. Kabla somo halijaanza, andika herufi kwenye ubao (changanya herufi kubwa na ndogo) ambazo wanafunzi wanasoma sasa hivi. 4. Kwa uchache unaweza kutumia herufi 4, lakini kinadharia tumia herufi 12 – 16. 5. Angalia mfano kwenye zoezi la kuchangamsha katika moduli hii. 6. Hakikisha herufi zinaonekana vizuri ili kufanya darasa zima lizione 7. Pitia Jina – neno kuu – sauti kwa herufi ulizochagua kutumia katika mchezo.	**Fanya mapitio kwenye herufi**
MAARIFA MAPYA	**5**	8. Waambie wanafunzi kwamba wanakwenda kushiriki kuunganisha sauti za herufi kwenye herufi zilizoandikwa kwa kucheza mchezo. 9. Tenganisha darasa katika makundi mawili (unaweza ukaligawa darasa kwa kufuata usawa wa katikati ya chumba). 10. Waambie wanafunzi kwamba mwakilishi mmoja kutoka kila timu atakuja mbele ya chumba kutambua herufi ambayo inatengeneza sauti husika. 11. Chagua wanafunzi wawili kuanza, mmoja kutoka kila timu. Wakaribishe kwenye ubao na mpe kila mmoja rula.	**Sikiliza ufafanuzi wa mwalimu juu ya Onesha Herufi**
KUIMARISHA MAARIFA	**10**	12. Waambie wanafunzi kwamba utatamka sauti ya mojawapo ya herufi zilizoko kwenye ubao na kwamba wanafunzi wanapaswa kushindana kuonesha herufi inayoendana na sauti hiyo. (Kama hauna uhakika na sauti za herufi, jambo ambalo ni sawa, waambie wanafunzi utasema neno ambalo linaanza na mojawapo ya herufi zilizoko kwenye ubao. Halafu watapaswa kushindana kuonesha herufi inayoendana na mwanzo wa sauti ya neno hilo.) 13. Wanafunzi wa mwanzo kuonesha herufi wanapaswa pia kuzalisha neno ambalo linaanza na herufi hiyo. 14. Kama amefanya kwa usahihi anakuwa ameipatia timu yake alama. Kama hayuko/hawako sahihi, wanafunzi wengine wana fursa ya kuonesha kwenye herufi sahihi na kutamka neno sahihi. 15. Mara tu wanafunzi wawili wakimaliza, waambie wachague kati yao mchezaji mpya kutoka kwenye timu na acheze tena kwa kutumia sauti ya herufi mpya. 16. Endelea hadi wanafunzi wote wapate zamu au hadi muda ukiisha.	**Fanya mazoezi ya kuunganisha sauti za herufi kwenye herufi zilizoandikwa**

KUPANGA MKAKATI

(Zunguka uangalie kama walimu wanahitaji msaada)

KUPANGA MKAKATI

MCHAKATO WA UFUNDISHAJI

HATUA	MUDA	VITENDO VYA UFUNDISHAJI	VITENDO VYA KUJIFUNZA
KUTUMIA MAARIFA	**15**	17. Unaweza kulifanya zoezi hili kuwa la juu zaidi kwa kuandika maneno badala ya herufi moja moja kwenye ubao. 18. Andika maneno kwa ukubwa wa kutosha kwa ajili ya wanafunzi kuona na kuweka kisanduku kuzunguka kila moja ili kutofautisha moja kwa nyingine. 19. Ikiwa wanafunzi wanaojitolea katika kila timu wako tayari, sema: "Tafuta neno ambalo linaanza na sauti /__/" AU "Tafuta neno ambalo linaishia na sauti /__/" 20. Yeyote atakayeonesha neno sahihi kwanza ameshinda alama kwa ajili yake au timu yake	**Fanya mazoezi ya kuunganisha sauti za herufi kwenye herufi zilizoandikwa**
UPIMAJI	**10**	21) Tilia mkazo sauti za herufi ambazo wanafunzi walikuwa hawazielewi vizuri 22) Rudia kufundisha sauti hizo katika madarasa yanayofuatia	**Unganisha sauti ya herufi kwenye herufi iliyoandikwa**

Tathmini: _____

Maoni: _____

UTENGENEZAJI WA ZANA ZA KUFUNDISHIA

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa tutaanza kufundisha utengenezaji vifaa wa moduli hii. Tutachukua jukumu la kusoma sehemu inayofuata kwa sauti. Baada ya mwalimu wa kwanza kumaliza aya, anaweza kumuita mwalimu mwingine kwa jina ili naye asome aya inayofuata”.

UTENGENEZAJI WA ZANA ZA KUFUNDISHIA

KUTENGENEZA MABANGO YA ALFABETI (DAKIKA 45)

Mabango ya Alfabeti ni moja ya vifaa vizuri kuwa navyo darasani kwa ajili ya maelekezo ya kusoma. Mabango ya alfabeti ni rahisi kutengeneza, yanaweza kutundikwa darasani, na yanaweza kutumika kwa ajili ya shughuli tofauti na mbalimbali.

Unaweza kutumia mabango ya alfabeti, pamoja na kadi picha ambazo ulitengeneza kwenye kipindi kilichopita, kuwafundisha, mbinu ya herufi – neno kuu – sauti.

Kutengeneza mabango ya alfabeti, unapaswa kuwa na vifaa vifuatavyo:

VIFAA VYA KADI YA PICHA	
√	Vipande vyenye ukubwa wa A4 vya karatasi ya manila – walau vipande 24 (jaribu kuwa na vipande 19 katika rangi moja (kwa konsonanti) , na vipande 5 katika rangi nyingine (kwa irabu), kama inawezakana)
√	Kama hauna karatasi ya manila, tumia bodi kadi au karatasi nyeupe
√	Mkasi
√	Vieweka alama au Mkaa
√	Kamba



HATUA YA 1:
Katika kila kipande cha karatasi, andika mfumo wa herufi ndogo na kubwa kwa kila herufi moja
⟶ Fanya hivyo kwa herufi zote 24 za Kiswahili (usihusishe herufi mwambatano – isipokuwa kwa 'ch'). Kama unafundisha darasa la 1, siyo muhimu kujumuisha herufi kubwa.



HATUA YA 2:
Kata kipande kirefu cha kamba ⟶ Inapaswa kuwa ndefu sana ili herufi zote 24 (vipande 24 vya karatasi vya A4) ziweze kuunganika, moja baada ya nyingine.

HATUA YA 3:
Tengeneza matundu madogo mawili kwenye kona za juu kushoto na kulia mwa kila kipande cha karatasi ⟶ Unaweza kutumia mkasi kutengeneza matundu.

UTENGENEZAJI WA ZANA ZA KUFUNDISHIA

WAAMBIE WALIMU:

" Tunaendelea kusoma matini kwa sauti na kwa kupokezana."

UTENGENEZAJI WA ZANA ZA KUFUNDISHIA

HATUA YA 4:
Penyeza kamba kupita katika matundu ⟶ Hakikisha herufi za alfabeti ziko kwenye mpangilio sahihi, na halafu hakikisha kwamba kamba inapita nyuma ya kadi herufi na kwenda nje kupitia katika kila tundu. Njia ya haraka ya kupitisha kamba kwenye herufi ni kukunja polepole herufi katika nusu na kupenyeza kamba kupita kwenye kadi herufi nyingi kwa mara moja (angalia chini).





HATUA YA 5:
Nyanyua bango la alfabeti juu kwa kuweka mwisho wa kila kamba mahali fulani katika darasa ⟶
Unaweza kufunga alfabeti yote au herufi ambazo zinasomwa tu. Kama inawezekana, nyanyua bango katika umbali au kimo ambacho kitamfanya kila mwanafunzi aone.

HATUA YA 6:
Shiriki katika kufundisha mfuatano wa herufi – neno kuu – sauti ⟶
Tumia kadi picha zako na bango jipya la alfabeti, fanya mchezo wa herufi – neno kuu – sauti kwa kufuata hatua zilizo katika moduli hii.

UTENGENEZAJI WA ZANA ZA KUFUNDISHIA

WAAMBIE WALIMU:

“Ukishamaliza bango alfabeti lako, jaribu kuigiza ukiwa na mwenzako. Jifanyeni mnafundisha herufi – neno kuu- sauti, kwa wanafunzi wenu”

WAAMBIE WALIMU:

“ Tunaendelea kusoma matini kwa sauti na kwa kupokezana.”

UTENGENEZAJI WA ZANA ZA KUFUNDISHIA

IGIZO (DAKIKA 10)

Pamoja na mwenzako, jifanyeni kuwa mwalimu na mwanafunzi. Fanyeni zoezi la kuwafundisha mbinu ya herufi – neno kuu – sauti kwao:

1. Tamka herufi na onesha herufi hiyo kwenye bango la alfabeti.
2. Tamka neno kuu na nyanyua juu kadi picha inayoendana na herufi hiyo
3. Tamka sauti ya herufi ambayo inaendana na herufi hiyo na onesha kwenye midomo yako.

UFUATILIAJI

Baada ya kujifunza moduli hii, mratibu elimu kata, afisa elimu wa wilaya, pamoja na wakaguzi watafuatilia kuona jinsi unavyotumia ujuzi uliopata katika ufundishaji wako darasani. Ni vizuri uwe tayari kwa ufuatiliaji huo kwa kuandaa:

- Kueleza kuhusu dhana ya foniki
- Kuonesha kwa vitendo sauti za herufi kwa herufi zote za alfabeti za Kiswahili
- Kutamka majina ya herufi kwa herufi zote za alfabeti za Kiswahili (siyo alfabeti za Kiingereza)
- Kuonesha kwa vitendo masomo mawili tofauti ambayo yanasaidia mwanafunzi kuunganisha sauti za herufi kwenye herufi zilizoandikwa.

MWISHO

WAAMBIE WALIMU:

"Walimu, tumefika mwisho wa moduli yetu, tumia dakika kumi kutafakari somo letu la leo. Jaza fomu kurekodi tathmini yako ya moduli. Baada ya kukamilisha chomoa ukurasa huo unipatie. Tafadhali uwe mkweli katika majibu yako kwa sababu yatasaidia kuboresha Mafunzo ya Walimu Kazini ngazi ya shule hapo baadaye."

Kusanya fomu za tathmini zilizokamilishwa na walimu na uwe nazo wakati wa mkutano mwingine katika kundi la kata.

Wakati walimu wanaendelea kujaza fomu za tathmini, tafadhali tafakari kwa ujumla juu ya mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika kipindi cha siku hiyo na jaza visanduku vinavyofuata. Haya utaweza kuyajadili pamoja na Timu ya Wilaya ya Mafunzo Walimu Kazini na Waratibu wengine wa Mafunzo Walimu Kazini wa mkutano unaofuata katika kundi la kata.

MAFANIKO YA JUMLA YA KIPINDI HIKI:	CHANGAMOTO ZA JUMLA ZA KIPINDI HIKI:

Shule: _____ **Wilaya:** _____ **Mkoa:**_____

Tafakuri za Moduli # _____ **Mada ya Moduli:** _____

Idadi ya walimu walioshiriki : _____ **Mwalimu Mkuu alishiriki : Ndiyo/Hapana**

MWISHO

MWISHO (DAKIKA 10)

Binafsi jaza fomu ifuatayo kuweka rekodi ya tathmini ya moduli ya leo. Baada ya kukamilisha, chomoa ukurasa huu na umpe Mratibu wako. Tafadhali uwe mkweli kwa vile mrejesho wako utasaidia kuboresha Mafunzo ya Walimu Kazi ngazi ya shule hapo baadaye.

JEDWALI LA KUTATHMINI			
Alama 0: Sikubaliani kabisa na usemi huu	**Alama 1: Kwa kiasi Sikubaliani** na usemi huu	**Alama 2: Nakubaliana kwa kiasi** na usemi huu	**Alama 3: Nakubaliana Kabisa** na usemi huu

FOMU YA TATHMINI

Shule: _____ **Wilaya:** _____ **Mkoa:**_____

Tathmini ya Moduli: _____ **Mada ya Moduli:** _____

Idadi ya walimu walioshiriki: _____ **Mwalimu Mkuu alishiriki: Ndiyo/Hapana**

Mratibu alikuwepo kuwezesha: Ndiyo/Hapana

Soma semi zifuatazo kisha weka alama ya vema katika kisanduku husika kuonesha jibu lako:	**0**	**1**	**2**	**3**
1. Dhana kuu ya moduli ya leo ilikuwa inaeleweka.				
2. Moduli hii ina mikakati mingi mizuri na yenye manufaa ambayo nitaitumia darasani kwangu.				
3. Muda uliotumika kukamilisha moduli hii unafaa. Sikuhisi kwamba ni muda mrefu sana.				
4. Moduli hii iliibua mjadala wa kufurahisha na tafakuri ya hali ya juu sana.				
5. Violezo vya kipindi cha kusoma na kuandika vilisaidia sana. Natarajia vitakuwa rahisi kuvitumia ndani ya darasa langu.				
6. Zana tulizotengeneza leo zitakuwa za manufaa sana (kama inahusika).				
7. Mratibu amejiandaa kwa kipindi – amesoma vizuri moduli na ameandaa vifaa vyote vya kufundishia.				
8. Mratibu anasimamia vizuri majadiliano – anajua jinsi ya kuwafanya watu wajieleze na namna ya kupata majibu.				
9. Mratibu anajua namna ya kusimamia makundi – anahakikisha kuwa walimu wanatoa ushirikiano, wanashirikiana na wana hamasika.				
10. Mratibu anajua jinsi ya kuwahamasisha walimu – anafuatilia kujua waliokosa vipindi au kuchelewa na kutukumbusha kwanini Mafunzo ya Walimu Kazini ni muhimu kwetu.				